

NOVENA KWA BIKIRA MARIA KICHANGA KITAKATIFU(30 AGOST -07 SEPTEMBER)

Mpenzi kichanga Maria, uliyeandaliwa kuwa Mama wa Mungu na Mama yetu bora na mpendevu, kwa neema za ajabu unazotupatia, kwa huruma usikie maombi yangu nikuombayo kwa unyenyekevu. Kutokana na shida na taabu zinazonisonga kutoka pande zote, na hasa katika taabu yangu ya sasa, ninaweka tumaini lote kwako. Ee kichanga kitakatifu, kwa neema ulizojaliwa peke yako, na kwa heshima ambayo umepewa, unionee huruma mimi leo. Nioneshe kwamba kisima au chanzo cha neema za kiroho na mafaaf mengine endelevu unayotugawia, hayaishi kwa sababu nguvu zako zilizoungana na Moyo wa Mungu, hazina ukomo. Kubali kupitia wingi wa neema zako ambazo Mwenyezi Mungu amekutajirisha tangu kuchukuliwa kwako mimba kwa kukiingwa dhambi ya asili, unijalie, Ee kitoto cha mbingu, ombi langu, na nitakusifu milele kwa wema na uzuri wa moyo wako. (Taja hitaji lako kwa Maria Kichanga Kitakatifu.....)

Baba Yetu x3, Salaam Maria x3 Atukuzwe Baba x3

MARIA KICHANGA KITAKATIFU

Picha ya kimiujiza inayoheshimiwa katika Nyumba Mama ya Masista wa Upendo huko Milan (Italia).

Imefasiliwa na Fortunata R Masaka-Rozari Hai 08/09/2021